

MKATABA WA KUPANGISHA NYUMBA

KATI YA

MUSSA REMIGIUS MUSSA wa S.L.P 1545 Dodoma ambaye katika Mkataba huu atajulikana kama "**Mwenye Nyumba**". **Simu: 0692298886**

NA

RJ MUSSA CONSTRUCTION COMPANY LIMITED wa **S.L.P 1545** Dodoma, Tanzania – ambaye katika Mkataba huu atajulikana kama "**Mpangaji**". **Simu: 0739607777**

Mkataba huu unashuhudiwa kama ifuatavyo:-

1. Kwamba, Mwenye nyumba ana miliki nyumba iliyopo Nyumba Miatatu **KISASA** Jijini Dodoma.
2. Kwamba, Mwenye Nyumba ana nia ya kupangisha nyumba kwa ajili ya Makazi /Ofisi tu na sio vinginevyo katika Mkataba huu.
3. Kwamba, Mpangaji atapanga nyumba ya kuishi /Ofisi kwa muda wa miezi 36 tu kuanzia tarehe **01/01/2024** hadi tarehe **30/12/2026** kwa Kodi ya Shilingi **120,000/= (Laki Moja na Elfu Ishirini)** kila mwezi ambayo kwa miezi 36 yaani Miaka 3 itakuwa Tshs. **4,320,000/= (Milioni Nne Laki Tatu na Elfu Ishirini)** Kodi ambayo italipwa wakati wa kusaini Mkataba huu.

Mkataba huu unashuhudiwa na mwenye nyumba kama ifuatavyo:-

- a) Mwenye nyumba anaahidi kutomwingilia mpangaji kwa namna yoyote kwa muda wote wa upangaji isipokuwa kwa sababu maalumu na baada ya kutoa taarifa kwa mpangaji.
- b) Mwenye nyumba anaahidi kutoongeza kodi ya nyumba katika muda wote wa mkataba bila makubaliano na Mpangaji.

Masharti ya Upangaji.

1. Kampuni ya Rj Mussa Construction imepangishwa Nyumba inayomilikiwa na sehemu ya Wakurugenzi wake Bwana Mussa Mussa, Kampuni inapaswa kulipa kodi kwa Mkurugenzi bila kuchelewa na kwa muda muafaka .
2. Hairuhusiwi mpangaji kumpangisha mtu mwingine nyumba bila idhini ya mwenye nyumba.
3. Mpangaji ana wajibu wa kulipa umeme, maji kulingana na bill zitakavyokuwa zinakuja na kuchangia gharama za kusomba maji taka.
4. Usafi wa nyumba ni jukumu la mpangaji.
5. Kodi itapokelewa na mwenye nyumba tu na si vinginevyo.

HIVYO BASI; Pande zote mbili zimeweka Saini katika namna, tarehe na mwaka kama inavyoonekana hapa chini.

**UMESAINIWA na KUWASILISHWA na
MUSSA REMIGIUS MUSSA**

Leo hii tarehe **01 Mwezi 01 Mwaka 2024**

**UMESAINIWA na KUWASILISHWA na
RJ MUSSA CONSTRUCTION COMPANY
LIMITED**

Leo hii tarehe **01 Mwezi 01 Mwaka 2024**



MWENYE NYUMBA



MPANGAJI

Jina la Shahidi Mpangishaji: **CHARLES JOHN MAKWENYA**

Saini: Charles Makwenya

Jina la Shahidi Mpangaji: **SOMOE SAID**

Saini: S. Said